

# **VITABU VYA MANABII**

## **Kitabu 2**

**Mafundisho juu ya**

**YEREMIA na  
MACOMBOLEZO**

**ELEZO HAKI**

ISBN 0-88873-186-8

*Imprimé au Canada*

copyright © 1972 William MacDonald All Rights Reserved

# YEREMIA NA MAOMBOLEZO

## *Soma maneno haya*

Kitabu hiki cha mafundisho juu ya unabii wa Yeremia na Maombolezo ni kimoja cha vitabu vitatu vilivyoandikwa juu ya vitabu vingine vya Manabii katika Agano la Kale.

Kitabu cha kwanza ni juu ya unabii wa Isaya.

Kitabu cha tatu ni juu ya Ezekieli na Danieli.

Vizuri ujipatie na kusoma kitabu cha kwanza, ndicho kitabu juu ya Isaya kama usipokisoma bado. Kuna mafundisho ya faida sana ndani ya kurasa 3 kufika 11 za kitabu kile ambayo unahitaji sana kukusaidia kufahamu vitabu vyote vya manabii. Kwa ukurasa 11 wa kitabu kile unaweza kuona kwamba Yeremia alitabiri kwa wakati wa wafalme gani na kwamba alisema zaidi kwa watu wa Yuda.

Soma sura moja ya Yeremia kila siku pamoja na kitabu hiki kwani si faida kusoma kitabu hiki peke yake. Sharti ukisome pamoja na Biblia. Ni lazima vilevile kusoma ndani ya Biblia yako mashairi yote mengine ambayo kitabu hiki kinataja.

Kwa mwisho wa mafundisho juu ya sura nyingine utaona ulizo. Jaribu kujibu maulizo haya, kisha angalia kwa kurasa 34-35 kuona kama ulijibu vizuri.

## YEREMIA

### Tunaweza kugawa unabii wa Yeremia hivi:

- Sura 1 Mungu aliita Yeremia kuwa nabii.
- Sura 2-19 Mungu alisema atahukumu ufalme wa Yuda, na ya kwamba nyuma yake atarudisha Wayuda tena kwa inchi yao wenyewe. Hatujui kama Yeremia alitoea hotuba hizi kwa watu wa Yuda wakati gani.
- Sura 20-33 Mungu ataleta jeshi la askari kuharibu Yuda na Yerusalema.
- Sura 34-45 Nini ilitokea kwa wakati wa Yeremia:
- 1) Wababeli walikamata Yerusalema, sura 34-39.
  - 2) Maneno yaliyotokea katika inchi ya Yuda nyuma ya kushindwa kwa Yerusalema, sura 40-42.
  - 3) Wengine wa Wayuda walikwenda Misri, sura 43-44.
  - 4) Habari kwa Baruku, sura 45.
- Sura 46-51 Mungu alitangaza kwa njia ya Yeremia kwamba atahukumu mengine ya mataifa.
- Sura 52 Jeshi la Babeli liliharibu Yerusalema, kama Mungu alivyosema mbele.

Watu wengine wanaita Yeremia **nabii wa machozi**. Tutaweza kufahamu unabii wake vizuri kama tukikumbuga alitoea machozi mara nyingi na kama alitoea machozi kwa sababu gani.

Yeremia alikuwa mwana wa Hilikia, kuhani, hivi Yeremia alikuwa kuhani vilevile. Alikaa ndani ya mji mdogo ambao uliitwa Anatoti, ndani ya sehemu ya inchi pahali watu wa kabila la Benyamina walipokaa.

Yeremia alianza kuhubiri maneno ya Mungu kwa watu wa inchi ya Yuda wakati Yosia alipokuwa mfalme wao. Kwa wakati ule majeshi ya Asuria walikuwa wameshinda watu wa taifa la kaskazini, ndilo Israeli, na kuwafanyiza wafungwa wao. Ilikuwa miaka michache tu mbele ya kuharibiwa kwa ufalme wa Yuda.

Mungu alionyeshea Yeremia kwamba askari wa Babeli watapeleka watu wa Yuda kwa Babeli kama wafungwa na kuwaacha pale

kwa miaka 70 kwa sababu ya zambi zao. Mungu aliagiza Yeremia kujulisha Wayuda neno hili na kusema nao kutii watu wa Babeli. Lakini watu wa Yuda walisema Yeremia alikuwa adui wa inchi yake mwenyewe, wakajaribu kumwua.

Askari wa Babeli waliruhusu Yeremia kubaki inchini mwa Yuda wakati walipokamata Yerusalema, lakini walipeleka zaidi ya watu kwa Babeli kama wafungwa. Yeremia alikataza watu ambao walibaki katika Yudea wasikimbie kwa Misri kupata kusaidia, lakini walikataa kupokea maonyo yake. Walikwenda Misri na kulazimisha Yeremia kwenda pamoja nao. Basi Yeremia alikufa pale Misri.

Yeremia alisema watu wa Yuda watapelekwa kwa Babeli kama wafungwa na vilevile kwamba taifa la Babeli litaharibiwa nyuma ya miaka makumi saba na halafu watu wa Yuda wataweza kurudia inchi yao.

Hotuba tunazosoma ndani ya kitabu cha Yeremia hazifuatani kwa utaratibu namna Yeremia alivyoitoa. Vizuri tukumbuke neno hili wakati tunaposoma kitabu hiki.

## SURA 1

Kwanza tunasoma namna Mungu alivyoita Yeremia kuwa nabii na kumwagiza nini ilimpasa kufanya. Yeremia alikuwa kuhani kwa sababu baba wake alikuwa kuhani (sh. 1), lakini Mungu alimchagua kuwa nabii hata mbele ya kuzaliwa kwake (sh. 5). Mungu alimpa uwezo (mash. 6-9), na kumwagiza kutangaza ya kwamba adui wa Yuda watawashinda na kuharibu mji wao mkubwa, ndio Yerusalema, lakini Mungu atawarudisha tena kwa inchi yao toka Babeli (sh. 10).

Katika inchi ya Palestina mti mmoja, ndio mlozi, unatoa maua madogo mara moja nyuma ya mwisho wa wakati wa baridi. Maua haya ni kama alama kwa watu kwamba wakati wa baridi unakwishisha. Hapa Mungu alimpa Yeremia alama ya [fimbo ya mlozi], ili aweze kufahamu ya kwamba wakati itakapopasa Mungu kuharibu watu wake ulikuwa karibu (mash. 11-12). Sufuria yenye maji yaliyotokota ilikuwa mfano wa jeshi la Babeli ambalo litafika nyuma kidogo na kuumiza watu wa Yuda kama maji ya kutokota yanavyoweza kuumiza mtu (mash. 13-16). Mungu aliagiza Yeremia kutangaza neno lake kwa watu wa Yuda hata kama wasipopenda kulisikia. Aliahidi kumsaidia na kumlinda (mash. 17-19).

Mungu alichagua Yeremia wakati asipozaliwa bado. Hata mbele ya kuzaliwa kwetu vilevile Mungu alitujua na kukusudi tuweze kufanya maneno fulani katika maisha

yetu. Yeremia alifanya maneno ambayo Mungu alimwagiza kufanya hata kama ilikuwa matata kwaye. Angaliharibu faida ya maisha yake mwenyewe na kupoteza baraka ya Mungu kama asingalitii agizo la Mungu kwaye. Mungu ana shauri kwa maisha yetu, lakini ni lazima kwetu kumtii. Kama tukimwasi tutakosa baraka ya Mungu na maisha yetu hayatakuwa na faida.

*Mungu alichagua Yeremia wakati gani kuwa mtumishi wake?*

## SURA 2

Ndani ya sura 2 kufika 33 tutasoma hotuba nyingi za Yeremia juu ya hukumu ya Mungu ambayo itakuja. Sura 2 kufika 19 zinatujulisha kwamba ilikuwa lazima kwa Mungu kuhukumu Yuda kwa sababu ya zambi zao. Watu wa Yuda walipenda Mungu mbele (mash. 1-4), lakini walikuwa wamegeuka (mash. 5-7). Waliacha kutumikia Mungu na walianza kutumikia sanamu (mash. 8-13). Hawakuamini Bwana lakini waliomba watu wa Misri na Asuria kuwasaidia na kuwalinda (mash. 14-19). Waliendelea ndani ya zambi zao na kuzidi kuabudu sanamu (mash. 20-25), na Mungu aliwaambia kwamba sanamu zao zote hazitawasaida wakati wa matata (mash. 26-28). Watu walisema maneno mabaya juu ya Mungu na walikataa kumtii ao kurudi kwake. Waliua manabii yake, walikataa kufanya maneno aliyowaagiza kuyafanya na walimsahau (mash. 29-32). Walisema hawakutenda mabaya lakini Mungu alijua zambi zao na ukali wao na atawahukumu (mash. 33-37).

## SURA 3

Watu wa Yuda walitenda sawasawa walipenda Mungu, lakini kabisa kabisa walipenda sanamu, na Mungu alisema walikuwa kama kahaba (mash. 1-5). Watu wa Yuda walikuwa wenye zambi kupita watu wa Israeli kwa sababu waliendelea ndani ya zambi zao hata wakati Mungu alipokwisha kuazibu Israeli (mash. 6-10). Mungu aliagiza Israeli kwa njia ya Yeremia kutengeneza maneno yao na kuacha kuabudu sanamu (mash. 11-13). Aliahidi kurudisha watu wa Yuda kwa inchi yao na kuwafunganisha pamoja na watu wa Israeli tena, kama wakatii maagizo yake. Aliahidi vilevile kuwa pamoja nao na kukaa katikati yao (mash. 14-20). Halafu watu wa Israeli walikiriri zambi zao (mash. 21-25).

*Kwa nini Mungu alisema watu wa Yuda walikuwa wabaya kupita Israeli?*

## SURA 4

Masiya atafikia watu wale ambao waliachana na zambi zao na kugeuka kwa Mungu. Atabariki mataifa wakati atakapokuja (mash. 1-2).

Mungu alitaka kufariji watu wa Yuda, hivi aliahidi ya kwamba Masiya atakuja. Aliahidi mara nyingi ya kwamba Kristo Masiya atafika. Neno kubwa zaidi ambalo tuna-jifunza ndani ya Agano la Kale ni kwamba Kristo atakuja. Agano Jipya linatufundisha ya kwamba Kristo amefika kweli. Watu wanaweza kuokolewa kwa njia ya Bwana Yesu Kristo tu. Haya ndiyo mafundisho makubwa zaidi ya Biblia.

Bwana alisema tena na watu wa Yuda na kuwaagiza kujinye-nyekeza na kuwa na huzuni kwa sababu ya zambi zao, na kujitoa kwake (mash. 3-4). Kama wasipofanya hivi Mungu atatuma jeshi la Babeli kuingia inchi yao. Mfalme wa Babeli atakuja toka upande wa kaskazini (mash. 5-6), kama simba (sh. 7). Yeremia na watu wote walihuzunishwa juu ya habari hizi (mash. 8-10). Bwana alisema watu wa Babeli watakuja mbio sana kama upepo wa moto, na kama mawingu (mash. 11-13). Yeremia alisihi watu kuachana na zambi zao (mash. 14-18). Alikuwa na huzuni sana na kupata ugonjwa mwilini kwa sababu ya watu wa Yuda; neno hili linaonyesha kwamba alipenda watu wa kabila lake sana sana (mash. 19-22). Alikuwa na ono la inchi ya Israeli na namna itakavyoonekana nyuma ya kuharibiwa na adui (mash. 23-31).

## SURA 5

Bwana atasamehe watu wa Yerusalema kama hata mtu mmoja mwenye haki akipatikana mjini (sh. 1). Lakini watu wote walikuwa wamekwenda mbali na Mungu: watu masikini ambao walikuwa wajanga, na wakubwa vilevile (mash. 2-5). Jeshi la Babeli litakuja na kuwaondosha toka inchi yao wenyewe kama wafungwa (mash. 6-19). Bahari ilitii Bwana, lakini watu wa Yuda hawakumtii (mash. 20-29). Hata viongozi wa watu kwa maneno ya dini, manabii na makuhani, hawakufuata Mungu na watu wa inchi walifurahi kuwa na viongozi namna hii (mash. 30-31).

Mungu alibariki watu wa Yuda kupita taifa lo lote lingine. Alisema atawapa Mfalme mkubwa na kuwaponyesha toka mikono ya adui wao kama wakimtii. Lakini watu wa Yuda walikataa kutii Mungu hata wakati alipowaazibu

kwa zambi zao. Neno hili linahakikisha kwamba watu wote ni waovu na wamekosea Mungu.

*Watu wa Israeli walikuwa na macho na masikio; kwa nini basi hawakuweza kuona na kusikia (sh. 21)?*

## SURA 6

Askari wa Babeli walijitayarisha kukamata Yerusalema (mash. 1-5). Mungu alikuwa akileta Wababeli kupigana na Yuda kwa sababu watu wa Yuda walikuwa waovu na wenye jeuri (mash. 6-8). Vijana na wazee walikataa kusikiliza Neno la Bwana, na makuhani na manabii walifanya vivyo (mash. 9-15). Hawakufanya maneno ambayo yalipendeza Mungu, hivi alikataa kupokea zawadi zao na alichukia matoleo namna hii (mash. 16-21). Wababeli wataleta woga na huzuni nyingi wakati watakapokuja (mash. 22-26). Mungu atatuma taabu kwa Yerusalema; itakuwa kama moto ambao watu wanatumia kutenga vyuma vya bei ya damani na uchafu. Lakini taabu hii haitaweza kulazimisha watu kuchana na uovu wao kwa sababu walikuwa wamekwamana kabisa ndani ya zambi na kwenda mbali sana na Mungu (mash. 27-30).

*Mungu aliahidi kuletea watu wa Yuda salama na raha kama wakatii maagizo yake (sh. 16). Inatupasa sisi kufanya nini kwa wakati wa sasa ili tuweze kupata salama na raha rohani? Ona Matayo 11:28.*

## SURA 7

Sura hii ni habari Yeremia alizotoa kwa mlango wa hekalu pahali Wayuda walipokwenda kuabudu Mungu. Watu wa Yuda walifikili hawatapata matata kwa sababu walizania Mungu hataruhusu adui kuharibu hekalu (mash. 1-4). Lakini walikuwa wamechafua hekalu kwa njia ya kuweka sanamu ndani yake na askari wa Wababeli wataliharibu. Hema ya Mungu ilikuwa kwa Shilo mbele lakini pahali pale palikuwa pameharibiwa; hekalu litaharibiwa vivyo hivyo (mash. 5-15). (Hakuna habari ndani ya Biblia kuonyesha kama Shilo uliharibiwa namna gani. Labda uliharibiwa kwa wakati wa Waamuzi ao wa Samweli ao Saulo.)

Mungu anataka watu kumpenda na kumtii. Kama wasipofanya hivi atawahukumu hata kama wakichunga utaratibu wa dini na kumwabudu kwa pahali alipoagiza watu kumwabudu. Ataharibu pahali penyewe kama watu ambao wanamwabudu pale wasipompenda kweli wala kumtii.



Mungu alikataza Yeremia kuombea watu wa Yuda kwa sababu walikuwa wakiinama mbele ya sanamu ambayo iliitwa *malkia ya mbinguni*. Sanamu hii ilikuwa katika njia kubwa ya Yerusalema kwa wakati ule (mash. 16-20). Watu walikuwa wakitolea Mungu zabihu, lakini ingalikuwa vizuri kupita kama wangelikula vyakula hivi wao wenyewe. Mungu alitaka watu kumtii, si kutimiza desturi za dini tu (mash. 21-26). Ilipasa Yeremia kutoa machozi kwa sababu watu wa Yuda hawatageuka na kusikiliza maneno ya Mungu (mash. 27-29). Wengi wa watu wa Yuda watauawa kwa sababu walichafua hekalu la Mungu na kuua watu kwa njia ya kuwatoa kama zabihu kwa sanamu zao (mash. 30-34).

## SURA 8

Watu wengi katika Yerusalema walikuwa wameabudu jua, mwezi na nyota. Mifupa yao itaondoshwa kaburini na kuachwa kulala juu ya udongo kwa nuru ya jua, mwezi na nyota (mash. 1-3). Watu walikataa kurudi karibu na Bwana. Hata ndege wanajua wakati inapowapasa kurudia nyumba zao, lakini watu wa Yuda hawatarudi karibu na Mungu (mash. 4-7). Viongozi wa watu kwa maneno ya dini walijua sheria lakini walitenda mabaya, na manabii na makuhani walifanya vivyo (mash. 8-13). Watu waliona hukumu ya Mungu ikikaribia na hawakuwa na tumaini tena (mash. 14-15). Jeshi la Babeli lilikuwa likikaribia (mash. 16-17). Yeremia alitoa machozi kwa sababu ya taabu yote ambayo itapata watu wa Yuda, na Mungu alimjibu (mash. 18-19). Yeremia alitoa machozi tena ndani ya mashairi 20-22.

Mungu anapenda watu wote na hataki kuwahukumu kwa zambi zao. Hata hivi ni lazima kwake kuazibu watu ambao wanakataa kuacha zambi zao, lakini anapata huzuni wakati inapompasa kufanya hivi. Anataka watu wote kuachana na zambi zao ili aweze kuwabariki na kuwaokoa.

## SURA 9

Yeremia alikaa kutoa machozi kwa sababu watu walizidi kufanya zambi (mash. 1-6). Bwana atawahukumu (mash. 7-9); ataleta jeshi la Babeli kuharibu inchi yao (mash. 10-14), na watu wa inchi watakwendea inchi nyingine (mash. 15-16).

Watu wengine wanalipa wanawake kufikia pahali pa maziko na

kuombolea mtu ambaye alikufa. Hapa Bwana anasema na wana-wake hawa kuombolea Yerusalema wakati Wababeli watakapou-kamata (mash. 17-22). Haifai watu kujitegemea wenyewe hata wa-kiwa wenye akili, nguvu na mali; sharti wategemee Bwana tu (mash. 23-24). Mungu ataazibu watu wa Yuda na watu wa Mataifa vilevile kwa sababu ya roho zao ngumu (mash. 25-26).

*Kwa nini Yeremia alitaka kwenda kukaa jangwani? Ona shairi 2.*

## SURA 10

Yeremia alisema na watu kwamba sanamu hazikuweza kuwa-saidia (mash. 1-5), lakini Mungu mkubwa aliweza kufanya hivi vi-zuri sana (mash. 6-16). Watu wa Yerusalema walianza kwendea inchi nyingine, kama wafungwa (mash. 17-18). Yeremia alitoa ma-chozi kwa sababu ya kuharibiwa kwa Yerusalema kwa mikono ya Wababeli (mash. 19-22). Alisema kwa ajili ya watu wa Yuda wakati alipoomba Mungu kuwafundisha na kuua watu ambao waliwa-chukia (mash. 23-25).

## SURA 11

Yeremia aliwaambia watu wa Yuda kwamba Mungu hatawa-bariki wala kuwasaidia kama wasipomtii sawasawa na agano ambalo alifanya nao kwa njia ya Sheria (mash. 1-8). Walikuwa wa-mevunja agano hili kwa njia ya kutumikia sanamu (mash. 9-13), na kwa sababu hii walikuwa wamekokota hukumu ya Mungu juu yao wenyewe (mash. 14-17). Bwana alimwambia Yeremia kwamba watu wa mji ulioitwa Anatoti walikusudi kumwua yeye pamoja na jamaa yake (mash. 18-19) Yeremia aliomba Mungu na Mungu alimwambia ataazibu adui wake (mash. 20-23).

*Watu wa Anatoti walikusudi kuua Yeremia kwa sababu gani?*

## SURA 12

Yeremia aliuliza Mungu kwa sababu gani alikubali kwa watu waovu kugeuka matajiri na kusitawi kama watu wa Anatoti (mash. 1-4). Mungu alimwambia Yeremia kwamba watu wa Yeru-salema watakuwa adui wakali kupita wale wa Anatoti (mash. 5-6). Mungu atatoa Yuda na Yerusalema kwa mikono ya majeshi ya inchi nyingine (mash. 7-13), lakini si kwa milele. Mungu ataazibu

mataifa yale na kurudisha watu wake kwa inchi yao wenyewe (mash. 14-17).

### SURA 13

Mungu alisema watu wa Yuda watakuwa kama kipande cha nguo ambacho Yeremia alitumia kama mkaba. Alificha mshipi huu karibu na mto Furati nao uliharibika; nyuma yake aliurudisha kwake (mash. 1-11).

Mungu alitaka watu kufahamu maneno ambayo aliwambia, hivi mara nyingi alitumia kitu fulani kueleza maana yao wazi waweze kufahamu vizuri.

Yeremia alificha mshipi ndani ya mwamba kufika wakati ulipokwisha kuharibika. Neno hili lilionyeshea watu wa Yuda kwamba watapelekwa kwa Babeli na wengi wao watakufa pale, hata wale ambao walikuwa watu wa Mungu.

Watu walifikili ya kwamba walikuwa na mvinyo ya kutosha. Ilikuwa kweli, lakini mvinyo yenyewe ilikuwa namna nyingine; ilikuwa mvinyo ya gazabu ya Mungu (mash. 12-14). Mungu aliwagiza kugeuza mwenendo wao. Wasipofanya hivi atawaondosha katika inchi yao wenyewe (mash. 15-17). Watu wengine wataingia inchini na kukamata mfalme na mama wake na kupigana na miji kwa upande wa kusini wa inchi (mash. 18-19). Jeshi la Babeli litaharibu inchi na kuiacha bule kwa sababu ya zambi ya watu wa Yuda (mash. 20-27).

*Kwa sababu gani Mungu aliagiza Yeremia kuficha mshipi wake ndani ya pango la mwamba?*

### SURA 14

Mvua haitanyesha inchini mwa Yuda na watu watakosa vya-kula (mash. 1-6). Yeremia aliomba Mungu kusaidia watu wa Yuda (mash. 7-9). Mvua itakosa na watu hawatapewa vyakula lakini watakufa kwa sababu ya vita na njaa na magonjwa (mash. 10-12). Manabii wa uwongo walisema ya kwamba watu wa Yuda hawatapata matata lakini hawakusema kweli na watauawa wao wenyewe (mash. 13-16). Mungu alisema na Yeremia kutoa machozi kwa sababu inchi na miji ya Yuda itaharibiwa (mash. 17-18). Yeremia aliomba Mungu asiache watu wa Yuda kupata taabu (mash. 19-22).

## SURA 15

Mungu alikataza Yeremia kuombea watu wa Yuda kwa sababu hatasikia maombi yake. Atatuma magonjwa kwao na vita na njaa, na wataondoshwa toka inchi yao kama wafungwa (mash. 1-4). Itakuwa huzuni kuona watu wa Yuda wakiteswa hivi, lakini walikataa kutii Mungu, hivi ilipasa Mungu kuwaazibu (mash. 5-9). Yeremia alichukiwa na watu wa kabila lake mwenyewe kwa sababu hawakutaka kusikia habari za hukumu ya Mungu juu yao. Walimchukia hata kama aliwaombea (mash. 10-12). Mungu alijibu akasema watu wale watageuka watumwa (mash. 13-14). Yeremia alisema maneno ambao alifikili yeye mwenyewe, na alisema vilevile kwa ajili ya watu wachache katika Yuda waliopenda Mungu (mash. 15-18). Mungu alisema watu wale waliotii neno lake watarudishwa kwa inchi yao (mash. 19-21).

*Yeremia alikula Kitabu cha Mungu kweli kweli?*

## SURA 16

Mungu alikataza Yeremia kuoa mke kwa sababu inchi itaharibiwa na watu wengi watauawa (mash. 1-4). Sasa Mungu alisema haifai Yeremia kutoa machozi kwa sababu alikuwa Mungu ambaye ataazibu watu wa Yuda (mash. 5-9). Watu watauliza Yeremia kwa sababu gani Mungu atawaazibu. Ilipasa Yeremia kuwafahamisha kwamba wataazibiwa kwa sababu hawakutii Mungu lakini walitumikia sanamu (mash. 10-13). Mungu atarudisha watu wa Yuda kwa inchi yao kwa wakati wa kuja (mash. 14-15), lakini kwanza watu wa Mataifa ambao waliokaa karibu nao watawawinda na kuwakamata kama mtu anavyowinda nyama, ao kama mvuvi anavyokamata samaki, na Mungu atawaazibu kwa sababu ya zambi zao (mash. 16-18). Watu wachache watarudi kwa inchi yao wenyewe na watasifu Mungu na kukiri ya kwamba walikuwa wapumbafu kabisa wakati walipotumikia sanamu (mash. 19-21).

Mungu aliazibu watu wa Yuda kwa sababu walitumikia sanamu, lakini hakusahau agano ambalo alifanya na Abrahamu. Alirudisha wengine wa watu wa Yuda kwa inchi yao. Kwa wakati wa sasa wengi wa watu wa Israeli hawakai ndani ya inchi yao wenyewe lakini Mungu hakusahau ahadi ambayo alitolea Abrahamu na Daudi; atarudisha Israeli tena kwa inchi yao. Atawapa Mfalme, ndiye Bwana Yesu Kristo, na atawabariki.

## SURA 17

Wayuda watapelekwa kwa inchi nyingine kama wafungwa kwa sababu walitumikia sanamu (mash. 1-4). Gazabu ya Mungu itatupata sisi vilevile kama tukitegemea watu, lakini Mungu ataturbariki kama tukimtegemea yeye (mash. 5-8). Mungu alijua kwamba watu wanasema wongo kwa wenzao mara nyingi, na tunajaribu hata kujidanganya wenyewe. Atazibu watu wale wanaosema wongo kwa kujipatia mali (mash. 9-11). Yeremia alijua Mungu tu aliweza kusaidia taifa la Yuda (mash. 12-14). Watu walimwuliza kwa sababu gani hawajaazibiwa kama Mungu alivyosema (sh. 15). Yeremia alimwambia Bwana kwamba watu walikuwa wakimcheka, akaomba Bwana kufanya neno ambalo alisema atalifanya (mash. 16-18). Kisha Yeremia aliagiza watu kushika siku ya sabato na aliwaonya ya kwamba Mungu atawaazibu kama wasipotii agizo hili (mash. 19-27).

*Mioyo ya watu ni namna gani?*

## SURA 18

Yeremia aliwaambia watu wa Yuda kwamba Bwana alikuwa kama mtu ambaye anafanya vyombo toka udongo, ndiye mfinyanzi. Watu wa Yuda walikuwa kama chombo cha udongo ambacho Bwana alikuwa akitumika juu yake. Mfinyanzi anaweza kufanya kama anavyotaka na udongo na Mungu atahukumu watu wa Yuda kwa zambi zao (mash. 1-17).

Mungu alitumia mfano wa chombo cha udongo mikononi mwa mfinyanzi kuonyeshea watu wa Yuda kwamba alikuwa mkubwa kupita na mwenye uwezo kupita wao na aliweza kuwatendea namna alivyotaka. Kila mtu ameumbwa na Mungu na Mungu ana ruhusa kufanya neno lo lote analotaka na mtu yule. Hatuna ruhusa kuuliza Mungu kwa sababu gani anaacha maneno fulani kutupata. Ingetupasa kujitoa kwa Mungu ili aweze kutimiza mapenzi yake ndani yetu kwa sababu Biblia inatufundisha kwamba Mungu anatupenda na hataki kutuumiza. Anataka kutubariki.

Watu wa Yerusalema walifanya shauri kuua Yeremia kwa sababu aliwaambia Mungu atawaazibu. Walisema waliani maneno ambayo makuhani na manabii wao waliwaambia, na walifanya shauri kusema wongo juu ya Yeremia (sh. 18). Yeremia alisema ya kama alihuzunika kwa sababu alikuwa ameomba Mungu aliwaazibu (mash. 19-23).

## SURA 19

Chupa ya udongo ni mfano wa Yuda na Yerusalema (sh. 1). Yeremia aliivunja kuonyesha kwamba majeshi ya Babeli watakuja na kuua watu na kuharibu miji (sh. 10). Mungu aliagiza Yeremia kuwa na uhodari na kuwaambia viongozi na makuhani kwamba walitumikia sanamu na kuua watu kama sadaka kwa sanamu zao, na kwa sababu hii Mungu atawaazibu.

## SURA 20

Pashuri alikuwa msimamizi mkubwa hekaluni. Alipiga Yeremia na kumfunga mikono na miguu (mash. 1-2). Kesho yake alimfungua tena na Yeremia alimwambia ya kwamba azabu kali itampata toka Mungu, pamoja na jamaa yake na watu wa Yerusalema na Yuda vilevile (mash. 3-6). Yeremia alihuzunishwa kwa sababu ilimpasa kuwaambia watu maneno ambayo hawakupenda kusikia lakini Bwana alimsukuma kufanya hivi (mash. 7-18). Yeremia alitaka kuacha kuwaambia watu ya kwamba Wababeli watawafanyiza wafungwa, lakini hakuweza (sh. 9). Alisikia rafiki wake wakifanya shauri kumwumiza (sh. 10), lakini aliamini Bwana atamlinda (mash. 11-12). Mara nyingine Yeremia alifurahi na alisifu Bwana, lakini mara nyingine alikuwa na huzuni na angalifurahi kama asingaliziwa (mash. 14-18).

*Pashuri alipiga Yeremia kwa sababu gani?*

## SURA 21

Mfalme Zedekia alituma mtu mwingine, jina lake Pashuri vilevile, kuuliza Yeremia kama Bwana alisema nini juu ya jeshi la Babeli ambalo lilikuwa likikaribia Yerusalema (mash. 1-2). Yeremia alisema Mungu atasaidia Wababeli kupigana na watu wa Yuda. Watafungua mfalme pamoja na watu wote wa Yuda wasiowaua (mash. 3-7). Wababeli wataua watu wote ambao watapigana nao, lakini wataacha hai watu wale ambao watajitoe kwao (mash. 8-10). Yeremia aliagiza jamaa ya mfalme kuhukumu maneno ya watu kwa haki (mash. 11-12). Mungu aliita watu wa Yerusalema wenye kukaa katika bonde na aliwajulisha ya kwamba watauawa (mash. 13-14).

## SURA 22

Sura hii inapasha habari za wafalme wane wa Yuda:

1. Mungu aliagiza Zedekia kutenda yaliyo haki; kama asipofanya hivi inchi ya Yuda itaharibiwa na watu watapelekwa kwa inchi nyingine (mash. 1-9).
2. Bwana alisema juu ya Yoahazi, aliyeitwa Salumu hapa. Alipelekwa Misri kama mfungwa na alikufa pale (mash. 10-12).
3. Yoyakimu hakulipa watu waliojenga nyumba yake kubwa. Hakutenda yaliyo haki kama baba wake Yosia alivyofanya, hivi Mungu alisema watu hawatamlilia wakati atakapokufa. Watakokota maiti yake inje ya mji bila kumzika vizuri (mash. 13-19).
4. Yoyakinu aliitwa Konia hapa. Mungu alisema atakwenda Babeli kama mfungwa, na atakufa pale. Wazao wake hata mmoja hawatatawala kama wafalme juu ya kiti cha kifalme cha Daudi (mash. 20-30).

Mfalme huyu aliitwa Yekonia vilevile na tunaona katika Matayo 1:11 ya kwamba alikuwa mzazi wa Yosefu, mume wa Maria. Yosefu hakuwa baba wa Bwana Yesu kwa sababu mimba ya Maria ilikuwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu (Matayo 1:20). Bwana Yesu atatawala juu ya kiti cha kifalme cha Daudi, lakini hakuwa wa jamaa ya Yekonia.

Bwana Yesu alikuwa wa jamaa ya Daudi kwa njia ya Natana, si kwa njia ya Solomono. Alikuwa mzao wa Daudi, lakini si wa Konia. Tunaona hapa ya kwamba Mungu anatimiza Neno lake kabisa.

*Bwana aliita watu wote kusikia maneno yake kwa sababu gani?*

## SURA 23

Mungu alisema wachungaji, ndio watawala wa watu walikuwa wameanguka kwa sababu hawakulinda watu wa Mungu (mash. 1-2). Lakini Mungu atarudisha wengine wa watu wake kwa inchi yao na kuwapa watawala ambao watawalinda vizuri (mash. 3-4). Mungu atatuma Masiya kuwa Mfalme wao (mash. 5-6), na watu watajua Mungu kama yule aliyerudisha watu wake kwa inchi yao (mash. 7-8). Mungu alionyesha ya kwamba manabii wa uwongo walizini na kutenda maneno maovu mengi (mash. 9-15). Manabii hawa waliahidi ya kwamba watu watakaa na salama (mash. 16-17), lakini Mungu hakuwaagiza kusema hivi (mash. 21-22). Walisema na watu kuabudu sanamu na kusahau jina la Bwana (mash. 23-32). Walizarau maonyo ya Bwana wakati ilipowapasa kumsikiliza. Mungu atawaazibu kwa zambi hii (mash. 33-40).

Kuna watu wengi ambao wanasema wanahubiri maneno ya Mungu. Mara nyingi wanasema maneno ambayo yanapendeza masikio ya watu, lakini maneno haya hayapatani na Neno la Mungu. Tusifikili Mungu anasema maneno ya kutufurahisha kila mara. Watu wa Yuda walikuwa wakiasi Mungu, hivi Mungu alisema atawaazibu. Ni lazima kwetu kuweka roho sana juu ya kusikiliza Neno la Mungu hata wakati linapotuonyeshea zambi zetu na tusipofurahi juu ya maneno ambayo tunayasikia.

### SURA 24

Wengine wa watu wa Yuda walikuwa wafungwa katika Babeli na Mungu alisema walikuwa kama matunda mazuri. Zedekia alikuwa pamoja na wakubwa wake na watu katika inchi ya Yuda; walikuwa kama matunda mabaya. Mungu atarudisha wafungwa kwa inchi yao toka Babeli, lakini watu ambao walikuwa kwanza katika Yuda watakimbia na kuuawa.

*Tini nzuri zilikuwa mfano wa nini?*

### SURA 25

Kwa miaka 23 Yeremia alikuwa ameonya watu kwamba Mungu atawaazibu, na watu wengine wa Mungu walikuwa wamesema nao vilevile kuachana na zambi zao na kutii Mungu (mash. 1-7). Watu wa Yuda watapelekwa kwa Babeli kama wafungwa na watakaa pale kwa miaka 70 kwa sababu walikataa kusikiliza habari Mungu alizotuma kwao (mash. 8-14). Mungu aliagiza Yeremia kuwaambia watu kwamba gazabu yake itaangukia watu wa Yuda na watu wote wengine ambao watahindwa na jeshi la Babeli (mash. 15-33). Mwishoni Mungu ataazibu Babeli vilevile. Inchi ya Babeli inaitwa Sesaki ndani ya shairi 26. Wachungaji, ndio watawala wa watu watalia na nguvu kwa wakati wa gazabu ya Mungu (mash. 34-38).

*Mungu alisema watu wa Yuda watakuwa wafungwa katika Babeli kwa muda gani?*

### SURA 26

Mungu aliagiza Yeremia kusimama kwa kiwanja inje ya hekalu na kuwaambia watu kwamba Bwana ataharibu hekalu namna alivyoharibu Shilo mbele, kama wasipoachana na zambi zao na kuge-



uka kwa Mungu (mash. 1-6). Makuhani walikasirika pamoja na manabii wa uwongo na watu. Walisema wataumiza Yeremia (mash. 7-11), lakini Yeremia hakuogopa; aliwaambia tena maneno ambayo aliwaambia mbele (mash. 12-15). Halafu wakubwa na watu walisema Yeremia alikuwa akifanya yaliyo haki na wanaume wazee walikumbusha watu kwamba nabii Mika alikuwa ametangaza habari toka Mungu bila woga na hakuuawa (mash. 16-19). Labda wale wasiopenda Yeremia waliwaambia rafiki zake kwamba Yoyakimu alikuwa ameuuwa nabii jina lake Uria ambaye alisema maneno yale yale Yeremia aliyasema; ao labda mashairi haya yanatupasha wazi kwamba Yoyakimu alikuwa ameuuwa Uria (mash. 20-23). Basi Ahikamu aliweza kuponyesha Yeremia asife (sh. 24).

### SURA 27

Mataifa ambao walikataa kutumikia Babeli watageuka wafungwa na watumwa. Vifungo vinatumiwa kuzuiza mfungwa asipate njia kukimbia; na mtu anatia kongwa juu ya shingo za ngombe zake wakati anapowatumikisha kazi (mash. 2,11). Vifungo hivi na kongwa ni mfano wa watu walio wafungwa ao watumwa (mash. 1-11). Yeremia aliomba mfalme Zedekia kujitoa kwa jeshi la Babeli. Haifai Zedekia aamini manabii wa uwongo waliosema vyombo vya hekalu la Mungu vitarudishwa nyuma kidogo kwa inchi ya Yuda toka Babeli. Ndiyo, nyuma kidogo Wababeli wataondosha hata vyombo vingine ambavyo vilibaki kwanza katika Yerusalema (mash. 12-22).

*Yeremia aliweka vifungo na kongwajuu ya shingo yake kwa sababu gani?*

### SURA 28

Hanania alisema wafungwa katika Babeli watarudia Yuda mbele ya kutimia kwa miaka miwili, lakini alisema uwongo (mash. 1-4). Yeremia alisema angalifurahi kama masemo ya Hanania yangalikuwa kweli, lakini watu hawatarudi katika muda ule. Yeremia alikuwa ametia kongwa ya miti juu ya shingo yake kama mfano kuonyesha kwamba watu wake watageuka watumwa (27:2). Sasa Hanania alivunja kongwa hii, lakini Mungu alisema ataweka kongwa ya chuma juu ya watu, na watalazimishwa kutumikia mfalme wa Babeli. Hawataweza kuvunja kongwa ya chuma (mash. 10-14). Yeremia alimwambia Hanania alikuwa nabii wa uwongo na atakufa mwaka ule ule. Hanania alikufa kweli nyuma ya miezi miwili, ona mashairi 1 na 17.

Hanania alikuwa nabii wa uwongo. Alitangaza kwa-mba Mungu alisema maneno fulani ambayo hakusema. Ni zambi kuonyesha kwamba unasema kwa ajili ya Mungu wakati unapotangaza mawazo yako mwenyewe tu. Mungu aliazibu Hanania kwa njia ya kumwondolea uzima wake.

### SURA 29

Yeremia alituma barua kwa watu wa Yuda ambao walikuwa wafungwa katika Babeli na kuwaambia ya kuwa watabaki pale kwa muda mrefu (mash. 4-7). Ndani ya barua hii Yeremia alisema itawapasa kukaa katika Babeli kwa miaka 70, kisha watarudi kwa inchi yao wenyewe (mash. 10-14). Mungu ataazibu Wayuda wale ambao walikuwa waovu katika Babeli na ataazibu vilevile watu ambao walikuwa kwanza katika Yerusalema (mash. 15-19). Mungu ataazibu manabii wawili wa uwongo, Ahaba na Zedekia (mash. 20-23). Ataazibu Semaya vilevile, ambaye aliandika barua kwa kuhani katika Yerusalema na kumwagiza kutia Yeremia gerezani. Kuhani, ndiye Zefania, alionyeshea Yeremia barua ya Semaya (mash. 24-29), na Yeremia alisema jamaa nzima ya Semaya watauawa na Semaya atakufa mbele ya wakati watu wa Yuda watakapofunguliwa toka utumwa katika Babeli (mash. 30-32).

*Semaya alikasirikia Yeremia kwa sababu gani?*

### SURA 30

Yeremia alifariji watu wa Yuda ambao walikuwa wafungwa katika Babeli. Alisema watarudia inchi ya Yuda na Mungu atawalinda kwa wakati wa taabu kubwa ambayo itapata wazao wa Yakobo (mash. 1-11). Bwana ataponyesha maumivu yao hata kama yaki-onekana sawasawa hawawezi kupona (mash. 12-22). Bwana ataua vilevile watu waovu (mash. 23-24).

### SURA 31

Bwana alisema atarudisha watu wa Israeli vilevile. Walikuwa watu ambao walikaa kwa upande wa kaskazini wa Yuda na walikuwa wazao wa wana kumi wengine wa Yakobo (mash. 1-6). Wataoka pahali mbalimbali katika dunia nzima (mash. 7-9), na furaha nyingi; wataimba na hawatatoa machozi tena (mash. 10-14). Maana ya Rakeli akililia watoto ndiyo hii: huzuni itakuwa nyingi wakati Waisraeli watakapopelekwa Babeli kama wafungwa. Huzuni hii

itakwisha wakati watakapoachana na zambi zao na Mungu atakapowasamehe (mash. 15-20). Watu wa Israeli watarudi kwa njia ambazo zinaonekana wazi na watafikia Mutu mmoja, ndiye Kristo Yesu, na kukaa karibu naye (mash. 21-22).

Watu wa Yuda watarudia inchi yao na kujenga miji yao (mash. 23-26). Watu wengi watakaa tena katika Yuda na Israeli na Mungu ataazibu kila mtu kwa zambi yake mwenyewe (mash. 27-30).

Mungu atafanya agano jipya na watu wa Israeli na watu wa Yuda. Agano hili litakuwa namna nyingine na agano la sheria. Msingi wa agano hili utakuwa neema ya Mungu.

Mungu alisema atafanya agano jipya na watu wa Israeli na watu wa Yuda. Tunasoma maneno haya tena katika Waebrania 8:8-12. Agano Jipya hili linasimama juu ya neema ya Mungu kwa njia ya Bwana Yesu Kristo. Wale wanaotumainia Bwana Yesu wamepokea hata sasa baraka za agano hili (Waebrania 10:16-18).

Watu watageuka namna nyingine na watapenda kufanya yaliyo haki, na watu wote watajua Bwana (mash. 31-34). Agano hili litaendelea kwa muda mzima jua na mwezi na nyota zinapowaka (mash. 35-37). Watu watajenga Yerusalema tena (mash. 38-40).

*Kwa nini Matayo alitumia maneno ya Yeremia 31:15 katika Matayo 2:18?*

## SURA 32

Mfalme Zedekia alifunga Yeremia gerezani kwa sababu Yeremia alisema jeshi la Babeli watashinda vitani (mash. 1-5). Kwa wakati ule Mungu aliagiza Yeremia kununua shamba toka mtu wa jamaa yake, ndiye Hanameli. Shamba la Hanameli lilikuwa katika Anatoti karibu na Yerusalema, naye alikuwa amefika karibu na Yeremia na kumwomba kulinunua. Yeremia alimpa Baruku barua ambayo ilionyesha kwamba alikuwa amenunua shamba hili, akamwagiza kuichunga vizuri (mash. 6-15). Yeremia hakufahamu kwa sababu gani Mungu alimwagiza kununua shamba katika Anatoti kwa sababu aliona jeshi la Babeli likizunguka Yerusalema (mash. 16-25). Bwana alisema ataharibu Yerusalema kwa sababu watu wa Yuda walitumikia sanamu zao (mash. 26-35), lakini atarudisha watu wake tena kwa inchi hii na kuwabariki sana (mash. 36-41). Watu watanunua na kuuza mashamba na udongo

tena (mash. 42-44), hivi Yeremia ao wazao wake wataweza kutumika na barua hii kuonyesha kwamba alikuwa amenunua shamba lenyewe.

*Kwa nini Yeremia alinunua shamba la mtu mwingine wa jamaa yake?*

### SURA 33

Mungu alisema tena kwamba watu wa Israeli na watu wa Yuda watarudia inchi yao wenyewe (mash. 1-10). Watu watakaa ndani ya inchi yao na kuwa na furaha sana (mash. 10-11); na kutakuwa na kondoo wengi wakijilisha juu ya vilima (mash. 12-13). Na Masiya atakuja; hili ndilo neno lililo zuri zaidi (mash. 14-18). Agano la Mungu na Daudi halitakwisha ungali mchana na usiku zinafuatana duniani. Siku zote Mtu wa jamaa ya Daudi atakuwa Mfalme, na jamaa ya makuhani wataendelea daima kutumikia Mungu (mash. 19-26). Kristo atatimiza ahadi hizi, hivi hazitageuka kamwe.

### SURA 34

Askari wa Babeli walikuwa wakipiga vita na watu wa Yerusalema na Mungu aliagiza Yeremia kujulisha Zedekia ya kuwa watamfanyiza mfungwa na atakufa katika Babeli (mash. 1-7). Mfalme alilazimisha watu kukubali kufungua watu wote wa Yuda ambao walikuwa watumwa; alifanya hivi wakati jeshi la Babeli walipokuwa wakipiga vita na Yerusalema. Nyuma kidogo watu waliingiza watu hawa katika utumwa tena. Labda jeshi la Babeli lilikuwa limeondokea Yerusalema kwa muda mfupi. Mungu alisema bwana hawa wa watumwa watapewa uhuru: maana yake watauawa kwa vita, njaa na magonjwa (sh. 17). Watu wengine walikuwa wameua mwana-ngombe kuonyesha kwamba watatimiza mapatano yao kufungua watumwa wao, lakini nyuma yake walivunja mapatano yenyewe; watu hawa watakuwa kwa sababu ya zambi hii. Mfalme Zedekia na wakubwa wake watageuka wafungwa na askari wa Babeli watafika tena na kuharibu mji (mash. 8-22).

Ni neno kubwa kutoa ahadi na ni lazima kwetu kuitimiza. Ni zambi kubwa kutolea Mungu ahadi bila kuitimiza. Inapasa Mungu kutuazibu wakati tusipotimiza ahadi zetu.

*Watu wa Yerusalema waliua mwana-ngombe kwa sababu gani (sh. 18)?*

## SURA 35

Yeremia alitii agizo la Bwana wakati alipoomba jamaa ya Rekabu kufika hekaluni na wakati alipowapa mvinyo kunywa. Watu wa jamaa ya Rekabu walikataa kunywa mvinyo kwa sababu baba wao Rekabu aliwakataza kunywa mvinyo. Walikataa kujenga nyumba vilevile, na kupanda mbegu; walikataa kupanda vyakula shambani ao kuwa na shamba la mizabibu. Walikuwa kama wageni katika inchi ya Yuda. Watu wa Yuda walikuwa namna nyingine. Wazao wa Rekabu walitii baba wao, lakini watu wa Yuda walikataa kutii Mungu, hivi ilipasa Mungu kuwaazibu. Lakini jamaa ya Rekabu haitakosa mtu daima atakayebarikiwa na Mungu. (Yonadabu, mwana mmoja wa Rekabu, alisaidia Yehu kuharibu waabudaji Bali inchini mwa Israeli, 2 Wafalme 10:15-28).

## SURA 36

Bwana aliagiza Yeremia kuandika maneno yote ambayo alikwisha kuwaambia watu wa Yuda. Baruku aliandika maneno ya Yeremia, na nyuma ya mwaka mmoja aliyasoma mbele ya watu hekaluni (mash. 1-10).

Mikaya alisikia Baruku akisoma maneno ya Yeremia, akakwenda na kuwaambia wakubwa wa Yuda neno hili. Wakubwa waliita Baruku aje na kuwasomea maneno haya vilevile; kisha walimwambia Baruku vizuri yeye na Yeremia wajifiche (mash. 11-19). Wakubwa walikwenda na kumwambia mfalme Yoyakimu habari za maneno ya Yeremia ambayo Baruku alikwisha kuwasomea na mfalme aliwaagiza kuleta kurasa hizi kwake. Mtu mmoja, jina lake Yehudi, alisomea mfalme maneno haya. Basi nyuma ya kuyasikia mfalme alitwaa kisu, akakata karatasi zenyewe na kuzitupa motoni. Wakubwa waliomba mfalme asiteketeze hotuba hizi, lakini mfalme alifunga masikio, akateketeza karatasi zote. Alitafuta Baruku na Yeremia vilevile lakini Bwana hakumruhusu kuwapata (mash. 20-26). Basi Yeremia aliandika hotuba hizi tena na kuongeza maneno mengine ambayo yalipasha habari za mauti ya kuogopesha ya mfalme Yoyakimu (mash. 27-32).

Mufalme wa Yuda alifanya zambi kubwa na kuongeza ukubwa wa hukumu yake wakati alipoteketeza kitabu ambacho kilipasha habari za gazabu ya Mungu kwa watu wa Yuda. Hatuwezi kamwe kukimbia Mungu na tutaongeza tu mateso yetu kama tukijaribu kushindana naye.

*Kwa nini Yoyakimu aliteketeza kitabu Baruku ambacho alikiandika (sh. 23)?*

## SURA 37

Wababeli waliondokea Yerusalema kwa muda mfupi wakati jeshi la Misri walipofika kusaidia watu wa Yuda (mash. 1-5). Lakini Bwana alimwambia Yeremia kwamba askari wa Babeli watarudi na kuteketeza Yerusalema (mash. 6-10). Askari wa mfalme Zedekia walikamata Yeremia na kumfunga gerezani saa alipokuwa aki-ondokea mji kufanya kazi kwa yeye mwenyewe. Walisema Yeremia alikuwa akikimbia (mash. 11-15). Nyuma ya muda fulani mfalme Zedekia aliita Yeremia, akamwuliza kama Mungu alisema nini juu ya vita. Yeremia alimwambia na uhodari kwamba jeshi la Babeli litakamata mji na kufunga mfalme. Halafu Yeremia aliomba mfalme kumfungua toka gereza na mfalme alikubali kufanya hivi (mash. 16-21).

## SURA 38

Watawala waliweka Yeremia ndani ya shimo ambalo lilikwenda chini sana, lenye matope, kwa sababu Yeremia alisema na watu vizuri waondokee Yerusalema na kujitoa kwa jeshi la Babeli (mash. 1-6). Mmoja wa watumishi wa mfalme alikuwa rafiki wa Yeremia naye aliomba mfalme kumruhusu kuondosha Yeremia shimoni. Mfalme alikubali, hivi mtumishi huyu alitwaa kamba na vipande vya nguo, akavuta Yeremia na kumtoa katika shimo (mash. 7-13).

Mtu wa Etiopia alisaidia Yeremia kutoka katika shimo. Watu wa Yuda wangaliacha Yeremia kufa pale. Mara nyingi watu wa dini ni waovu na wakali sana. Mara nyingine Mungu anatumika na watu ambao hawaonekani kama watu wa Mungu lakini wanaopenda Mungu kupita watu wengi wa dini.

Mfalme Zedekia aliuliza Yeremia nini ilimpasa kufanya na Yeremia alisema naye kuacha kupiga vita lakini ajitoe kwa jeshi la Babeli. Wengine wa Wayuda walikuwa wamekwenda kufungana na jeshi la Babeli, lakini Yeremia alisema watu hawa hawatacheka mfalme (mash. 14-23). Zedekia aliomba Yeremia asimwambie watu habari za maneno waliyokwisha kuyasema katikati yao, lakini kusema tu ya kwamba aliomba mfalme asimrudishe gerezani (mash. 24-28).

*Kwa nini Ebedimeleki alitupa vitambaa vilivyoharibika chini kwa Yeremia ndani ya shimo (sh. 11)?*

## SURA 39

Mwishoni, jeshi la Babeli walikamata Yerusalema. Mfalme Zedekia, wana wake na askari wake walijaribu kukimbia, lakini Wababeli waliwakamata. Waliua wana wa mfalme, wakaondosha macho ya mfalme na kumpeleka kwa Babeli kama mfungwa. Wababeli waliacha inchini mwa Yuda watu wachache tu ambao walikuwa masikini sana (mash. 1-10).

Maneno ambayo Mungu anasema yanatimizwa kila mara. Yereimia alimwambia Zedekia kwamba askari wa mfalme wa Babeli watamfunga kama akikaa kupiga vita (34:2-6; 38:18). Zedekia hakuamini Mungu na hakuamini neno lake, hivi aliteswa kama kipofu na mfungwa katika Babeli. Ni akili kwa sisi kuamini Neno la Mungu na kufanya maneno ambayo anayasema. Kama tusipofanya hivi tutapata matata.

Nebukadneza, mfalme wa Babeli, alifanyiza Gedalia mtawala wa Yuda, akamwagiza kutendea Yereimia mema (mash. 11-14). Bwana aliahidi vilevile kulinda Ebedimeleki (mash. 15-18). Ebedimeleki ndiye mtumishi wa mfalme ambaye aliondosha Yereimia shimoni.

## SURA 40

Wababeli waliuliza Yereimia kama alitaka kubaki katika Yuda ao kwenda Babeli. Yereimia alichagua kubaki inchini mwa Yuda (mash. 1-6). Mtu mwovu, jina lake Isimaeli alifanya shauri kua Gedalia, mtawala wa Yuda. Watu walimwambia Gedalia ya kwamba Isimaeli alitaka kumwua, lakini Gedalia hakuamini masemo yao, na alikataa kufunga Isimaeli gerezani (mash. 7-16). Misipa ulikuwa mji mkubwa wa Yuda kwa wakati inchi ya Yuda ilipotawaliwa na Wababeli (sh. 6).

*Yohana alimwambia Gedalia nini?*

## SURA 41

Isimaeli na watu wake waliua Gedalia. Labda walimwua kwa sababu alikuwa akitii watawala wao, ndio Wababeli, ao kwa sababu walitaka kutawala inchi wao wenyewe (mash. 1-3). Isimaeli aliua vilevile watu 70 ambao walifika kwa Misipa kuabudu na alitupa miili yao ndani ya shimo kubwa udongoni (mash. 4-10). Yohana aliponyesha watu wengine ambao waliweza kukimbia Isima-

eli; walikimbia kwa Betelehemu wakitaraji kuondoka tena kule kwenda Misri (mash. 11-18).

### SURA 42

Yohana na watu ambao walikuwa pamoja naye waliogopa, wafika karibu na Yeremia kuuliza kama Bwana alitaka wafanye nini (mash. 1-6). Iliwapasa kukimbia kwenda Misri, ao kubaki katika inchi ya Yuda? Bwana alisema atawasaidia kama wakibaki katika inchi ya Yuda, lakini wakikwenda Misri, watakufa wote kule (mash. 7-22).

*Watu wa Yuda walitaka kweli kweli kujua mapenzi ya Mungu?*

### SURA 43

Yohana alimwambia Yeremia kwamba alikuwa akisema wongo, kisha alipeleka Yeremia na Baruku na watu wote waliokuwa pamoja naye kwa Misri (mash. 1-7).

Watu wa Yuda walikuwa wameteswa kwa sababu walikataa kutii Mungu na walitumikia sanamu. Askari wa Babeli walikuwa wameua wengi wao na kupeleka wengine kwa Babeli kama wafungwa. Watu wachache wa Yuda waliachwa ndani ya inchi yao, lakini hata hivi walikataa kuanini Mungu na kufanya maneno ambayo aliwaagiza kufanya. Mungu alisema, "Mkae inchini mwa Yuda na nitawalinda ninyi pale. Mtakufa kama mkikwenda Misri." Lakini walikataa kusikia na kutii Mungu; wakakwenda Misri, wakakufa pale kama Mungu alivyosema.

Kwa Misri Yeremia alikuwa ndani ya mji ambao uliitwa Tapanesi, na Bwana alimwagiza kuficha mawe makubwa ndani ya udongo wa matofali katika tanuru, kwa mlango wa nyumba ya Farao, mfalme wa Misri. Kisha Mungu alimwambia Yeremia kwamba Nebukadneza, mfalme wa Babeli, atapiga vita na Misri na kushinda Wamisri na kusimamisha kiti chake cha kifalme kwa pahali Yeremia alipoficha mawe ndani ya udongo wa matofali katika tanuru (mash. 8-13).

### SURA 44

Pale kwa Misri Yeremia aliwaambia watu wa Yuda kwamba Mungu alikuwa amewaazibu kwa sababu walitumikia sanamu



(mash 1-6), tena waliendelea kuabudu sanamu hata katika Misri (mash. 7-10). Mungu atawafanyiza wote kufa kwa sababu walikuwa wakitumikia sanamu; hakuna mmoja wao atakayerudia inchi ya Yuda (mash. 11-14). Lakini watu wa Yuda walikataa kusikiliza Yeremia. Walisema hawakupata matata wakati walipotumikia sanamu (mash. 15-19). Yeremia alisema nao Mungu alituma taabu hii kwao kwa sababu walitumikia sanamu (mash. 20-23), na ya kwamba hawakuweza kuomba Mungu kwa sababu ya zambi yao. Mungu atawaazibu, na majeshi mengine watakuja na kushinda Misri, inchi ambayo waliitegemea (mash. 24-30).

Sura hii inatupasha juu ya Yeremia katika Misri. Hatusomi tena habari nyingine juu ya Yeremia; tunafikili alikufa katika Misri.

*Watu wa Yuda waliabudu mungu mke gani katika Misri?*

## SURA 45

Yeremia aliandika sura hii wakati Yoyakimu alipokuwa mfalme wa Yuda, hivi maneno ambayo tunasoma ndani ya sura hii yalitokea mbele ya maneno ndani ya sura 44. Hapa Yeremia alifaraji Baruku wakati Baruku alipokuwa na huzuni sana. Yeremia alisema Mungu alitenda kwa haki wakati alipobariki ao kuazibu watu ao inchi. Vizuri Baruku asijitafutie mambo makubwa na asiyatafute kwa watu wa Yuda vilevile.

*Kwa nini Yeremia alikataza Baruku kujitafutia mambo makubwa hapa duniani?*

## SURA 46

Mungu anajua maneno ambayo yatapata mataifa na inchi hata wakati maneno haya yasipotokea bado. Tunajua Biblia ni kweli na ni Neno la Mungu. Mungu alijulisha manabii yake maneno ambayo yatatokea nao waliandika habari hizi. Na kweli maneno haya yalitokea namna Mungu alivyosema. Ndani ya sura 46 kufika 49 tunasoma maneno mengi ambayo Mungu alisema yatapata watu wa makabila mengine waliokaa karibu na watu wa Yuda. Maneno haya yalitokea kweli na yanatokea hata sasa namna Mungu alivyoonyesha mbele.

Sura hii inatupasha juu ya Misri na sura 47 kufika 51 zinapasha habari za maneno ambayo yatapata mataifa mengine. Wakati Nebukadneza asipofika bado Yeremia alisema atashinda jeshi la Misri kwa Karkemisi. Nabii alisema juu ya majeshi wakijitayarisha kwa

vita; watu wa Misri walijivuma na walifikili watashinda, lakini watu wa Babeli walishinda watu wa Misri (mash. 2-12). Yeremia alisema na watu wa Misri kujitayarisha kwa kuja kwa Nebukadneza ambaye atawapeleka kwa inchi yake kama wafungwa (mash. 13-24). Mungu ataazibu watu wa miji ya Misri, lakini nyuma atawarudisha tena kwa inchi yao (mash. 25-26). Mungu atarudisha Waisraeli vilevile kwa inchi yao, lakini si kwa wakati ule (mash. 27-28).

### SURA 47

Jeshi la Babeli litakuja toka kaskazini na kushinda Wafilistini. Litawazuiza wasipate kusaidia toka miji ya Tiro na Sidona na litharibu miji ya Wafilistini vilevile

### SURA 48

Sura hii ni juu ya watu wa Moabu. Mungu atawaharibu kwa sababu walijitegemea wenyewe. Walitumikia sanamu na kukaa katika usitawi na furaha za dunia na walizarau na kucheka watu wa Israeli. Jeshi la Babeli litafika gafula kama ndege mkubwa, kama tai, na kuwameza (sh. 40). Hata hivi Mungu atasimamisha watu wa Moabu tena wakati Kristo atakapokuja kutawala (sh. 47).

*Wamoabu waliharibiwa kwa milele?*

### SURA 49

Waamoni walikuwa wenye kiburi na walifikili wao ni watu wakubwa; Mungu atawaazibu, lakini hawatauawa wote (mash. 1-6).

Watu wa Edomu walifikili walikuwa wenye akili na ya kwa- mba hakuna jeshi ambalo litaweza kuwashinda kwa sababu walika milimani, lakini Mungu alisema watauawa wote (mash. 7-22).

Mungu alijulisha watu wa Damasiki katika Suria ya kwamba mji wao utaharibiwa. Vijana wataanguka njiani na kufa, na askari wote watauawa (mash. 23-27).

Jeshi la Babeli wataua watu wote wa Arabia ambao walikaa katika Kedari (mash. 28-29).

Nebukadneza na majeshi yake watakamata mji jina lake Hazori na kuondosha mali yake yote na vitu vyote vya mali na kuacha mji bule nyuma ya kuuharibu (mash. 30-33).

Watu wa Elamu watalazimishwa kuhangaika duniani, lakini Mungu atawarudisha tena wakati Bwana atakapokuja (mash. 34-39).

### SURA 50

Sura hii na sura 51 zinaonyesha namna gani Mungu atahukumu watu wa Babeli. Watu toka kaskazini, ndio Wamedi, watashinda Babeli (mash. 1-3).

Mungu alitumika na watu wa Babeli kuazibu watu wake Yuda kwa zambi zao. Lakini Wababeli walifanya zambi kubwa kupita Yuda, hivi Mungu alitumika na watu wa taifa lingine kuazibu Wababeli.

Mungu anaazibu watu kwa zambi zao naye anaazibu vilevile mataifa kwa zambi za watu wao.

Yeremia alisema Mungu ataazibu Babeli, na nyuma yake alisema mara sita kwamba watu wa Yuda na Israeli watabarikiwa. Baraka ya kwanza ni ndani ya mashairi 4-7. Adui watahinda Babeli na kuondolea watu wa Babeli mali yao, hata kama Babeli ilikuwa kama mama wa mataifa mengine (mash. 8-16). Mungu atarudisha watu wa Israeli na kuwasamehe (mash. 17-20). Yeremia alipasha habari za gazabu ya Mungu juu ya Wababeli (mash. 21-32) na ya kwamba alikumbuka watu wa Israeli na Yuda (mash. 33-34). Watu wa Babeli watauawa vitani, na jeshi la Wamedi litaharibu mji wa Babeli na kuuacha bule. Watu wa inchi nyingine watasikia kwamba jeshi la Wamedi lilikuwa limeharibu mji wa Babeli (mash. 35-46).

*Mungu aliita Wababeli "nyundo" kwa sababu gani (sh. 23)?*

### SURA 51

Mungu atatuma mtu kuharibu Babeli bila rehema (mash. 1-4). Neno hili linaonyesha kwamba Mungu hakusahau watu wa Israeli na Yuda (sh. 5). Mji wa Babeli ulikuwa mji wa utajiri, lakini Mungu atatumika na majeshi ya Wamedi kuuharibu (mash. 6-14). Mungu ni mkubwa kupita sanamu zote; Mungu wa kweli ndiye Mungu wa Israeli na Yuda (mash. 15-19).

Mungu alisema na Wamedi (mash. 20-23), na ni kama ndani ya shairi 24 alikuwa akisema na watu wa Yuda. Kisha alisema na watu wa Babeli tena (sh. 25). Mlima wa uharibifu ni watu wa Babeli. Mji wa Babeli utatekwa na kuachwa bule kwa milele na hakuna mtu ambaye atakaa tena pale. Zaidi ya nyumba na kuta zitavunjwa na nyama wa poli tu watakaa pale (mash. 25-37). Yeremia alisema juu ya karamu kubwa ambayo Belsasari, mfalme wa Babeli ataitayari-

sha (mash. 38-40). (Majeshi ya Wamedi walikamata Babeli usiku ule ule, kama tunavyosoma ndani ya Danieli 5.) Bahari (sh. 42) ni jeshi la Wamedi walioingia mji wa Babeli na kuondosha vitu vyote vya faida (mash. 41-44). Mungu alisema na Wayuda ambao walifungwa katika Babeli na kuwaagiza kuondokea mji mbele ya kufika kwa Wamedi. Waliagizwa kungoja kufika wakati mfalme mpya atakapowafungua tena (mash. 45-51). Jeshi la Wamedi watashinda mji wenye kiburi, ndio Babeli, watafunja kuta zake na kunyamazisha masemo yote ya kiburi ya watu wa mji (mash. 52-58).

Mbele ya ile Yeremia aliagiza Seraya kupeleka kitabu pamoja naye wakati atakapopeleka kwa Babeli kama mfungwa. Kitabu gani? Kitabu chenye maneno ya Mungu juu ya kuanguka kwa Babeli. Seraya aliagizwa kusoma kitabu hiki kwa watu, kisha kukifunga pamoja na jiwe na kukitupa ndani ya mto Furati. Neno hili lili onyesha kwamba mji wa Babeli utaharibiwa (mash. 59-64).

## SURA 52

Tunasoma tena juu ya siku za mwisho za maisha ya mfalme Zedekia (mash. 1-11), na juu ya kuharibiwa kwa Yerusalema (mash. 12-16). Halafu Yeremia alisema juu ya sahani na vyombo vya hekalu ambavyo askari wa Babeli walikwenda navyo (mash. 17-23). Kiongozi wa jeshi la Wababeli alileta watu 74 toka Yerusalema karibu na mfalme wa Babeli. Mfalme aliwaua wote kwa Ribla (mash. 24-27). Wengine wa watu wa Yerusalema walipeleka kwa Babeli kama wafungwa (mash. 28-30). Mfalme wa Babeli aliondosha Yoyakinu, mfalme wa Yuda, gerezani, nyuma ya kukaa pale kwa miaka 36, na alimlinda vizuri kufika siku ya kufa kwake.

Mungu ni mwenye haki naye anaazibu watu ambao wanamkosea. Mungu ni mwenye mapendo vilevile na anatendea mema watu ambao wanatubu wakati wanapozibiwa na wale wanaoomba Mungu kuwasamehe. Mungu alifanyiza mfalme mkali wa Babeli kutendea Yoyakinu mema hata alimwondosha gerezani na kumchungu vizuri.

*Yoyakinu alikuwa na miaka mingapi wakati mfalme wa Babeli alipomwondosha gerezani?*

# MAOMBOLEZO YA YEREMIA

*Ona sehemu za kitabu hiki:*

1. Mji wa Yerusalema ulikuwa mtupu kwa sababu uliharibiwa, 1:1-11.
2. Maombi ya watu wa Yerusalema, 1:12-22
  - 1) Watu walilia, mash. 12-17.
  - 2) Watu walikiri zambi zao, mash. 18-19.
  - 3) Watu waliomba Mungu, mash. 20-22
3. Bwana ndiye aliyeazibu Yerusalema, 2:1-22.
  - 1) Neno lililotokea kwa sababu ya gazabu ya Mungu, mash. 1-13.
  - 2) Sababu ya gazabu ya Mungu — alikasirika kwa sababu manabii wa uwongo hawakuonya watu, sh. 14.
  - 3) Watu wengine walitazama maneno ambayo yalikuwa yakitokea na walizarau watu wa Yerusalema, mash. 15-16.
  - 4) Mungu aliazibu Yuda kama alivyosema atafanya, sh. 17.
  - 5) Nabii aliwaambia watu vizuri wawe na huzuni kwa sababu ya zambi zao na kuziacha, mash. 18-19.
  - 6) Yeremia aliomba Mungu kuwa na rehema, mash. 20-22.
4. Nabii alisema kwa ajili ya watu wa Yuda walioachwa. Alisema walijua walikuwa wametenda zambi na ya kwamba walikuwa na huzuni juu ya zambi yao, 3:1-66.
  - 1) Mungu aliazibu watu wa Yuda, mash. 1-18.
  - 2) Rehema ya Bwana, mash. 19-39.
  - 3) Watu walikiri ya kwamba walikuwa wamefanya zambi, mash. 40-47.
  - 4) Yeremia alikuwa na huzuni kwa sababu Yerusalema uliharibiwa, mash. 48-51.
  - 5) Nabii aliomba Mungu kumlinda watu wasipate njia kumwua, mash. 52-66.
5. Nabii alionyesha kwamba watu wa Yuda walikuwa wamegeuka kabisa, 4:1-20.
6. Maneno ambayo yatatokea kwa wakati wa kuja. Watu wa Edomu watauawa, lakini watu wa Yuda watarudi tena, 4:21-22.

**7. Watu ambao waliamini waliomba Mungu kuwarehemu na walimwomba kuwarudisha tena kwa inchi yao, sura 5**

Watu wa Yuda waliteswa sana sana wakati majeshi ya Babeli walipokamata Yerusalema. Mateso na maumivu yao yalisukuma Yeremia kuandika kitabu hiki cha Maombolezo. Ni kitabu cha kulia na machozi na Yeremia alikiandika wakati alipoona mji wa Yerusalema ukivunjwa na kuharibiwa, na watu wengi wakiuawa.

Ndani ya kitabu cha Yeremia tuliona hotuba za nabii juu ya maneno ambayo yatatokea nyuma kidogo. Kitabu hiki kidogo cha Maombolezo kiliongezwa juu ya kitabu cha Yeremia. Kinaonyesha ya kwamba Yeremia alitoa machozi wakati Yerusalema na hekalu la Mungu yalipoharibiwa. Hakufurahi kwa sababu unabii wake ulitimizwa. Alihurumia watu ambao walikuwa wakiteswa na aliwambolea.

Kitabu cha Maombolezo kinaonyesha nini Yeremia alisikia rohani mwake, pamoja na maneno haya mengine:

1. Kinatupasha kwamba watu wengine wa Yuda walikuwa na huzuni wakati walipoona jeshi la Babeli likifika. Yeremia alisema kwa ajili yao.
2. Kinatuonyeshea kidogo maumivu na huzuni ya Kristo Masiya wakati alipofika hapa duniani na kuteswa na kufa juu ya msalaba wa Kalvari. Kwa mfano, Bwana Yesu angeweza kusema maneno kama yale ya shairi 12 la sura 1.
3. Kinaonyesha huzuni ya Wayuda ambao watafuata Bwana kwa wakati wa kuja saa watakapoteswa kwa muda wa Mateso Makubwa. Wakati huu unaitwa vilevile wakati wa taabu ya Yakobo.

Sura 1, 2 na 4 za Maombolezo ni namna nyingine na maandiko mengine. Kila sura ina mashairi 22 na kila shairi linaanza na herufi nyingine ya Kiebrania, kwa namna zinavyofuatana ndani ya alfabet. Sura 5 ina mashairi 22 vilevile, lakini herufi kwa mwanzo wa mashairi haya hazina utaratibu fulani.

## SURA 1

Hapa tunaona ya kwamba Yerusalema uliharibiwa kabisa na watu hawakukaa tena ndani yake. Sanamu hazikusaidia watu wa Yerusalema. Mataifa mengine walisema watawasaidia lakini waliwageukia (mash. 1-2). Watu wa Mungu walikuwa wamefanya zambi na hivi askari wa Wababeli waliwapeleka kwao kama wafungwa. Watu wa Yuda hawakufikia Yerusalema tena kutumikia

Mungu (mash. 3-9). Wababeli walikuwa wameondoa vyombo vya zahabu na vya feza vya hekalu (sh. 10), na vyakula havikutosha kwa watu waliobaki inchini (sh. 11). Watu wa Yuda walitoa machozi na kukiri zambi zao (mash. 12-19), na waliomba Mungu kuwarehemu na kuua adui wao (mash. 20-22).

Watu wa Yuda walikuwa wamekosea Mungu naye aliwaazibu kwa zambi zao. Watu wengi wa inchi nyingine walifanya zambi kupita watu wa Yuda, lakini Mungu aliazibu watu wake mwenyewe kwanza. Watu wa Yuda walikuwa watu wa Mungu na walijua ya kwamba Mungu aliwapenda. Alikuwa amewapa sheria zake nao walijua maneno gani yaliyo haki. Mungu aliwaazibu kwanza kwa sababu aliwapenda na alitaka kuwafundisha kuachana na zambi zao na kuishi kwa yeye.

*Kwa nini Mungu aliazibu watu wake mwenyewe mbele ya kuazibu watu wengine?*

## SURA 2

Mashairi haya yanaonyesha maneno ambayo Mungu aliyate ndea watu wa Yuda na inchi yao. Aliharibu hekalu lililoitwa kiti cha miguu yake hapa (sh. 1). Aliharibu miji (sh. 2). Hakuzuiza adui wasifike (sh. 3); na hakulinda hata hekalu lake. Watu hawakuweza kuleta tena nyama kutoa kama zabihu ndani ya hekalu na Mungu aliondoa wafalme na makuhani (sh. 6). Watoto njiani walikuwa zaifu kwa sababu walikosa vyakula, wakaanguka na kufa (mash. 1-12). Masumbuko ya watu yalikuwa makubwa sana hata Yeria hakuweza kuwafaraji wala kuwafurahisha (sh. 3). Wengine wa mama walikuwa na njaa sana hata walikula watoto wao wenyewe (sh. 20).

## SURA 3

Hapa Yeria alisema kwa ajili ya watu wa Yuda. Mungu aliwakasirikia sana (mash. 1-18). Waliweza kutumainia rehema yake tu (mash. 19-33). Mungu alitenda kwa haki wakati alipowaazibu kwa zambi zao (mash. 34-39). Kisha Yeria aliomba watu kukiri zambi zao na kuziacha na kujitoa kwa Bwana na kumwomba kuazibu adui wao (mash. 40-66).

*Watu walifikili ya kwamba Mungu hakuwapenda tena?*

## SURA 4

Yeremia alisema kwamba mbele Yerusalema ulikuwa mji mzuri sana na wa kushangaza, lakini sasa ulikuwa tupu. Askari wa Babeli walivunja hekalu na mama wengine walikwenda zao na kuacha watoto wao peke yao (mash. 3-4). Wengine walikufa kwa sababu walikosa vyakula (sh. 5), na wengine waliteswa kwa wakati mrefu (sh. 6). Wakubwa walionekana sawasawa na watu wengine tu (mash. 7-8). Wengine wa wanawake walikuwa na njaa sana hata walikula watoto wao wenyewe (sh. 10). Watu walifikili hakuna mtu ambaye ataweza kuingia mji, lakini Wababeli walikuwa wameuharibu (sh. 12). Taabu hii kubwa ilikuwa tunda la zambi za manabii na makuhani na watu (mash. 13-16). Walitaraji jeshi la Misri litafika kuwasaidia, lakini Misri haikuwasaidia hata kidogo (sh. 17). Jeshi la Babeli liliwafikia gafula (mash. 18-19) na kufanyiza mfalme Zedekia mfungwa wao na kumpeleka kwa Babeli. Zedekia anaitwa hapa mpakaliwa wa Bwana (sh. 20). Watu wa Edomu walifurahi wakati Wababeli walipokamata Yerusalema, lakini Mungu atazibu watu wa Edomu na kujenga tena Sayuni, ndio Yerusalema (mash. 21-22).

Mungu aliazibu watu wa Yuda kwanza, kwa sababu walikuwa watu wake naye aliwapenda. Aliazibu watu wa Edomu kwa sababu yeye ni Mungu wa watu wote na inchi zote. Anaazibu watu wote wanaotenda mabaya. Labda haazibu watu ao inchi nyingine mara moja wakati wanapofanya zambi kubwa, lakini hata hivi anaazibu zambi zote kwa wakati wa kutimia. Hataacha hata zambi moja bila kuazibu mwenye kuitenda.

*Watu wa Misri ao wa Edomu walisaidia Waisraeli kwa wakati wa taabu yao?*

## SURA 5

Ndani ya mashairi 1 kufika 18 watu walitoa machozi kwa sababu ya taabu ambayo waliipata. Walilia kwa sababu vyakula na vitu vyote vilikuwa na bei gali (sh. 4); iliwapasa kutumika kazi bila kupata mishahara (sh. 5); bwana wao wa kazi walikuwa wakali (sh. 8); watu masikini walikuwa na njaa na walikaa na woga (mash. 9-10); bwana wao waliwatendea maneno ya kuogopesha sana makali kabisa (mash. 11-12). Kisha watu waligeuka kwa Bwana na kumwomba kuwarehemu (mash. 19-22).

*Maandiko ya Yeremia yametuonyeshea ya kwamba Mungu anapenda watu wake. Aliwaambia kwamba atawa-*



*hukumu kama wasipoachana na zambi zao. Yametuonyeshea vilevile ya kwamba Mungu ni mtakatifu na anachukia zambi. Aliazibu watu wa Yuda kwa zambi zao. Yeria alitoa machozi wakati alipoona taabu na maumivu ambayo yatapata watu wa Yuda. Mungu anahuzunishwa vilevile na kuumia rohoni wakati watu wanapokataa kuachana na zambi zao na inampasa kuwaazibu.*

*Tuombe Mungu kutupa sisi roho ya toba kwa zambi zetu wenyewe. Tuwe na roho ya huruma vilevile kwa watu wengine na kuwaombea na kuwasaidia kuacha njia ya uharibifu na kurudi kwa Bwana, kwa utukufu wake na baraka yao wenyewe.*



# *Majibu kwa Maulizo*

## *YEREMIA*

### **Sura**

- 1 Mbele ya kuzaliwa kwake (sh. 5).
- 3 Kwa sababu watu wa Yuda waliona namna Mungu alivyoa-zibu Israeli, lakini hata hivi walikataa kuachana na zambi zao (mash. 7,10).
- 5 Kwa sababu mioyo yao ilikuwa miovu na hawakutaka ma-neno ya Mungu (sh. 23; Marko 8:17-18).
- 6 Kuja kwa Bwana Yesu.
- 9 Watu wote wa Yerusalema walikuwa wenye zambi na Yere-mia alitaka kuondoka karibu nao.
- 11 Kwa sababu aliwaambia maneno ya Mungu.
- 13 Neno hili lilikuwa mfano wa maneno Mungu ambayo atate-ndea Yuda.
- 15 Maana ya shairi 16 ndiyo hii: Yeremia alipokea maneno ya Mungu na kufikili na kufurahi juu yao.
- 17 Ni miovu sana (sh. 9).
- 18 Mungu anaweza kufanya neno lo lote analotaka na watu (sh. 6).
- 20 Kwa sababu Yeremia alikuwa amesema Mungu ataharibu Yerusalema (19:14-15).
- 22 Alitaka kusema neno kubwa sana, ndilo hili: wazao wa Konia hawatakuwa wafalme wa Israeli (sh. 30).
- 24 Watu wa Yuda waliokuwa wafungwa katika Babeli.
- 25 Miaka 70 (sh. 7).
- 27 Kama alama ya kwamba watu wengi watakuwa wafungwa katika Babeli.
- 29 Kwa sababu Semaya hakuamini kwamba Mungu alikuwa amesema na Yeremia (sh. 27).
- 31 Kwa sababu Herode aliuu watoto wadogo wote katika Yeru-salema (Matayo 2:16).
- 32 Kwa sababu Mungu alimwambia adui watakwenda zao na watu wa Yuda wataweza kuwa na mashamba tena (sh. 15).
- 34 Kuonyesha ya kwamba watatimiza ahadi yao na kufungua watumwa wao.
- 36 Hakuogopa Mungu wala kumheshimu.
- 38 Kusudi kamba zisiumize Yeremia wakati watu walipomvuta toka shimo.
- 40 Ya kwamba Isimaeli atajaribu kumwua (mash. 13,15).
- 42 Sivyoy, walikuwa wamefanya shauri kwenda Misri (sh. 20).

- 44 Malkia ya mbingu (sh. 25).  
45 Kwa sababu Mungu atahukumu watu wote (sh. 5).  
48 Sivyoy, Mungu atarudisha watu wa Moabu wakati Bwana Yesu atakapokuja tena (sh. 47).  
50 Kwa sababu walikuwa wamevunja mataifa mengi mengine.  
52  $20 + 11 + 37 =$  miaka 68 (mash. 1,3).

### *MAOMBOLEZO*

#### Sura

- 1 Taifa la Israeli walikuwa na sheria ya Mungu na walijua Mungu kupita mataifa mengine.  
3 Sivyoy. Walijua Bwana aliwaonyeshea rehema mpya kila asubui (sh. 23).  
4 Sivyoy; Wamisri hawakuweza kuwaokoa (sh. 17), na Wamedomu walifurahi (sh. 21).